

Ndugu Mzazi:

Karibu kwenye program ya mafunzo ya awali ya Jumuiya ya Cedar Rapids! Tungependa kukutambulisha kwenye idara yetu ya afya na kukupatia maelezo machache kuhusu ofisi yetu katika shule ya mtoto wako. Kutakua na nesi wa shule na msaidizi wake katiki kipindi chote cha masomo. Msaidizi wa nesi amefuzu mafunzo ya Huduma za kwanza na CPR na katika utoaji dawa.

Vitu vifuatavyo vinahitajika kikamilika na kuletwa shuleni ili mtoto aweze kuhudhuria

- **Cheti cha chanjo (saini kadi)** - Sheria ya Iowa inalazimu chanjo za mtoto kabla ya kuanza shule ya awali (au labda serikali ikupe kibali)
- **Rekodi ya mihani wa kimwili (physical Exam)** - Inajika uwe na karatasi ya uchunguzi wa mwili iliyoandikwa na kusainiwa kabla ya kuanza chekechea.
- **Kibali cha kuruhusu huduma za mtoto za HACAP** - Hii fomu ni ya kutoo kibali kwa HACAP kutoa huduma ya uchunguzi wa masikio kwa watoto wote wa chekechea katika mwaka wa masomo.
- **Cheti ya ukaguzi wa meno** - Ijapokuwa, fomu hii haiitajiki, ila tunapendekeza mtoto wako awe amefanyiwa uchunguzi wa meno kabla ya kuanza chekechea.
- **Cheti cha ukaguzi wa macho** - Ijapokuwa, fomu hii haiitajiki, ila tunapendekeza mtoto wako awe amefanyiwa uchunguzi wa macho kabla ya kuanza chekechea.
- **Chanjo zinaweza kupatikana:**
 - Doctor's Office
 - Linn County Health Department (319-892-6095)
 - Metro Care Connection (319-558-2481)
- **Uchunguzi wa mwili (physical exam) unaweza kufanyika:**
 - Mganga wa familia
 - Community Health Free Clinic (319-393-0416) huduma za afya za bure.
 - Metro Care Connection (319-558-2481) huduma za afya mashuleni.
 - Eastern Iowa Health Center (319-730-7300) huduma kulingana na kipato.
- Tunaelewa ya kwamba afya yam toto wako inachangia kwenye uwezo wake wa kujifunza. Kama mtoto wako ana tatizo Fulani la kiafya au anahitaji msaada, tafadhali wasiliana nasi, utaratibu wa kiafya unawezafanywa shuleni. Kwa mfano:
 - ◆ Asma
 - ◆ Kisukari
 - ◆ Kifafa
 - ◆ Anadhurika na kitu /nakuhitaji Epi-pen
 - ◆ Siko Sell
 - ◆ Matatizo ya kichwa/akili
- **Dawa Shuleni**
 - Mzazi/Mlezi ni lazima usaini fomu kutoa ruhusa ya mtoto wako kupatiwa dawa. Fomu hii ina[atikan katika ofisi ya afya ya shule au kwenye tovuti ya jumuiya ya mashule ya Cedar Rapids kabla mtoto wako hajapatiwa dawa.
 - Dawa zilizo andikwa na maganga lazima ziwe kwenye chupa yake na jina la mwanafunzi, daktarin liwe limeonyeshwa.
 - Dawa zilizonunuliwa lazima ziwe halali na saini kabla hazijatolewa shuleni. (hii nipamoja na dawa za kikohozi, Tylenol, Advil nk). Fomu ya kutoa ruhusa ya dawa vile vile inaweza kujazwa na kufaxiwa katika ofisi ya afya shule kutoka kwa aliyendika.

Nesi wa shule na Msaidizi wake watakuwepo kukusaidia and kumsaidia mtoto wako kadri itakavyohitajika. Tafadhali jisikie huru kuwasiliana nao kama una maswali yeyote. Tunasubiri kwa hamu kumsaidia mtoto wako. Kwa maelezo Zaidi tafadhali tembelea kwa mtandao wetu: <http://www.cr.k12.ia.us/departments-services/school-health-services/>